



Mwongozo kwa Vyombo vya Habari wa Kuwasiliana Wakati wa Dharura za Afya ya Umma



BBC
MEDIA ACTION

TRANSFORMING LIVES THROUGH MEDIA
AROUND THE WORLD

Waandishi

Genevieve Hutchinson na Jacqueline Dalton

Mbunifu

Lance Bellers

Picha ya jalada la mbele

Wanawake wakijadili chanjo ya pepo-punda wakati wa tukio la kufikia jamii la Madubi huko Nigeria.

SHUKRANI: BBC MEDIA ACTION

Yaliyomo

1 Utangulizi kwa huu mwongozo	4
2 Jinsi vyombo vya habari vinavyoweza kuleta utofauti	5
3 Dharura za afya ya umma ni zipi?	6
4 Jinsi ya kuokoa maisha: Mwongozo kwa mawasiliano	14
5 Vyanzo vya taarifa za ziada	30



I Utangulizi kwa huu mwongozo

Janga la afya ya jamii au dharura linaashiriwa na uwezo wake wa kusababisha afya dhoofu na vifo vya mamia, maelfu au wakati mwingine mamilioni ya watu.

Wakati wa janga la kiafya, vyombo vya habari vina nguvu ya kuokoa maisha.

Mawasiliano sahihi yanaweza kusaidia kuzuia au kupunguza usambaaji wa ugonjwa, na kuwaongoza wale waliothirika kufikia huduma za afya na tiba.

Huu mwongozo unatoa bakshishi kwa wataalamu wa vyombo vya habari juu ya jinsi ya kusaidia hadhira/watazamaji wakati wa dharura za kiafya.

Unaweza ukasomwa pamoja na mwongozo uliozalishwa na [BBC Media Action's Lifeline Production Manual](#) Lifeline (unapatikana mtandaoni) ambao unatoa maelekezo ya jumla ya jinsi ya kuwasiliana na watu walioathirika na majanga ya kibinadamu ili kusaidia kuokoa maisha na kupunguza mateso.¹

Dharura za afya ya jamii zinaweza kuanza haraka au taratibu sana.

**Hiki kitabu kitashughulikia zile zinazoanza kwa haraka:
Dharura za afya ya umma zilizoanza kwa haraka.**

Juu

Kufuatia mafunzo ya mawasiliano wakati wa milipuko, waandishi wa habari wa Idadu FM – Benin walitayarisha kipindi cha maswali na majibu kwa njia ya simu na wasikilizaji.

KWA HISANI YA: HADRIEN BONNAUD/UNICEF

¹ BBC Media Action (2013), *Lifeline programming for people affected by crises* (online). Available at: <https://www.bbc.co.uk/mediaaction/publications-and-resources/brochures/lifeline-programming>

2 Jinsi vyombo vya habari vinavyoweza kuleta utofauti

Mwitikio mzuri wa kimawasiliano kwa dharura ya afya unaweza ukawa na utofauti kati ya makumi au mamia ya watu wanaoathirika, au maelfu na mamilioni ya watu wanaoathirika.

Vyombo vya habari vinaweza kuwafikia watu kwa haraka zaidi na kwa upana, kuwaunganisha wananchi, wataalamu na waitikiaji wa dharura. Vinaweza kuwapa watu taarifa muhimu kutoka vyanzo vinavyoaminika ili wajue kinachoendelea, jinsi ya kujikinga, na lini na namna gani ya kupata matibabu na msaada. Vinaweza kusaidia kupunguza hitaji la wafanyakazi wa afya au wahamasishaji wa kijamii kusafiri kwenda kuinua uelewa juu ya dharura ya afya ya umma, hususan kwenye mazingira ambayo watu wanaweza kuwepo, au wanahitaji kuwepo na kutenganishwa ili kuzuia usambaaaji wa ugonjwa. Kupunguza madhara ya dharura ya afya hupunguza mzigo mkubwa kwa huduma za afya na pia kuokoa maisha zaidi.

Ukosefu wa taarifa sahihi na za kuaminika wakati wa dharura unaweza kuleta uvumi na taarifa za uwongo, kupelekea taharuki na machafuko, matendo ambayo yatawafanya watu wawe hatarini zaidi, na/au unyanyapaa kwa watu walioathiriwa na ugonjwa, vyote ambavyo vinaweza kuchangia watu wengi zaidi kuathiriwa au kufa wakati ugonjwa unasambaa. Mashirika ya vyombo vya habari yanaweza kusaidia kujaza pengo hatari la taarifa na kukabiliana na taarifa zisizo sahihi.

Pia kuna ushahidi kuwa vyombo vya habari vinaweza kucheza nafasi muhimu wakati wa majanga ya afya ya umma kwa kuwapa uhakika, kukuza utulivu na kuhamasisha watu kuchukua hatua ya kuboresha hali zao.²

² BBC Media Action (2015). Research report: Humanitarian broadcasting in emergencies – A synthesis of evaluation findings (online). Available at: <https://www.bbc.co.uk/mediaaction/publications-and-resources/research/reports/Humanitarian-broadcasting-in-emergencies-synthesis-report-2015>

3 Dharura za afya ya Umma ni zipi?

Janga au dharura ya afya ya umma inaashiriwa na tukio la kiafya lenye uwezo wa kusababisha afya dhaifu au ugonjwa, ulemavu na/au vifo kati ya idadi kubwa ya watu au asilimia kubwa ya watu.³

Kama dharura ya afya inakuwa kubwa inaweza kupelekea serikali kutangaza “hali ya hatari”, kuifanya kubadili kazi za mashirika ya taifa ili kusimamia muitikio wa dharura.⁴

Janga au dharura ya afya ya jamii inaweza kuwa tukio lililopo la haraka, kama mlipuko wa kipindupindu ndani ya kambi ya wakimbizi wakati wa majanga ya kibinadamu, au tukio lililopo la taratibu, kama kuongezeka kwa unene uliopindukia katika nchi nyingi. Kama ilivyotajwa kwenye utangulizi, hiki kitabu kinalenga matukio ya haraka ya majanga au dharura ya afya ya jamii.

Mlipuko ya magonjwa kwa kiwango kikubwa inaweza kuwa mzigo unaoelemea huduma za afya na kukanganya namna ya kawaida ya maisha, na kunaweza kukawa hakuna tiba au matibabu ya kawaida. Matumizi yaliyoshamiri ya safari za kimataifa inamaanisha pia mlipuko au janga unaweza kuwa ugonjwa mkubwa iwapo mwikio hautakuwa umeratibiwa vyema, kwa wakati na kwa usahihi.

Mifano ya magonjwa yenye uwezo wa kusababisha dharura ya afya ya jamii:

- **Kipindupindu** ni aina ya hatari ya kiafya ndani ya dharura za kibinadamu. Mlipuko wa Haiti miezi 10 baada ya tetemeko la ardhi la 2010 ilipelekea kesi za kipindupindu 600,000 zilizokadiriwa na vifo 7,436 ndani ya miezi 22. Msongamano, lishe duni, ukosefu wa maji safi, ukosefu wa miundombinu ya usafi, kuzidiwa kwa huduma za afya na umaskini ndio zilikuwa sababu kubwa ya kusambaa kwa kasi kwa Kipindupindu Haiti, na ndivyo ilivyo kwa mlipuko mingi ya ugonjwa huu.⁵

³ WHO (2017), *Emergency Response Framework* (online). Available at: <http://apps.who.int/iris/bitstream/handle/10665/258604/9789241512299-eng.pdf;jsessionid=2C902589AC35344B0A22D5C5868C976E?sequence=1>

⁴ WHO (undated), *Definitions: emergencies* (online). Available at: <https://www.who.int/hac/about/definitions/en/>

⁵ Townes, D (2018), *Health in Humanitarian Emergencies: Principles and Practice for Health and Healthcare*, Cambridge University Press

- **Mafua** kwa kawaida huwa ya msimu bali kuna wasiwasi kwamba ukosefu wa udhibiti makini na tahadhari za uangalizi unaweza kupelekea janga kubwa la mafua na mamilioni ya vifo ndani ya miaka kadhaa.⁶ Watu sita wenye mfumo dhaifu wa kinga, kama wanawake wajawazito, wazee na watoto chini ya miaka mitano wapo katika hatari fulani.

Kiwango kikubwa cha ugonjwa kinaweza kuwa mzigo unaoelemea huduma za afya na kuweka ulazima kwa familia na jamii kuwahudumia wale wanaoumwa; pia kuwaweka na wao hatarini. Mlipuko ambao unaathiri watu wengi kwa miezi au miaka unaweza kuwa na athari kubwa kwa sekta zingine; kwa vile watu wanashindwa kufanya kazi au kuhudhuria shule, kwa sababu wanaumwa au wanatunza wale wanaoumwa au wanajaribu kukwepa kuambukizwa ugonjwa.

- Mlipuko ya **magonjwa yanayodhibitika kwa chanjo** kama surua, homa ya manjano na ugonjwa wa kupooza hutokea kwa sababu ya taarifa za uwongo kuhusu chanjo; muktadha wa kibinadamu unaovuruga huduma za chanjo na uhamiaji mkubwa wa watu katika maeneo ambayo upatikanaji wake wa chanjo ni hafifu. Hii mlipuko ina uwezo wa kuwa dharura za afya ya umma kama kiwango cha chanjo hakitaongezeka.

Wakati wa muda wa kuandika hii (mwisho wa 2018), mlipuko wa ugonjwa wa kupooza unaendelea Nigeria, Afghanistan na Pakistan, na kumekuwa na mlipuko ya hivi karibuni katika nchi ambazo ugonjwa wa kupooza ulishamalizika (kama Somalia na Syria). Mlipuko wa surua Ulaya pia ni matokeo ya kushuka kwa viwango vya chanjo kutokana na taarifa zisizo sahihi.

- Mlipuko wa **virusi vya Ebola** wa mwaka 2014–2016 Afrika Magharibi ulisambaa kwa kasi ndani ya Sierra Leone, Liberia na Guinea, na kupelekea maelfu ya vifo. Wakati mlipuko mkubwa ukiwa ndani ya hizi nchi tatu, usafiri wa kimataifa ulipelekea kesi kadhaa za ugonjwa huu kuonekana katika nchi zingine, zikiwemo Mali na Nigeria. Ukiongezea vifo vilivyosababishwa moja kwa moja na Ebola wakati huo, vifo ndani ya Sierra Leone, Liberia na Guinea vilitokea sababu

⁶ WHO (2018), *Influenza* (online). Available at: <http://www.who.int/influenza/en/>

watu walikosa huduma za afya kwa ajili ya magonjwa mengine. Watu waliepuka huduma za afya kuliko kawaida kwa sababu huduma hizi zilielemewa, hazikuwa zikipatikana au sababu watu waliogopa kupata Ebola katika vituo vya afya.

Usambaaji wa kasi wa Ebola uliunganishwa na sababu kadhaa. Hizi zilijumuisha asili ya virusi, vitendo vya kitamaduni vya mazishi ambavyo viliwaleta watu kugusana na wengine walio na Ebola katika wakati ambao wanaweza kuambukiza zaidi, taarifa zisizo na ukweli ambapo ilimaanisha watu hawakupunguza kugusana na wengine mapema zaidi, makazi yaliyosongamana kwa baadhi ya maeneo, na kusafiri kwa walioathirika.

Maana

Maradhi: Hali yo-yote inayomsababisha mtu kujisikia vibaya. Hii inajumuisha magonjwa, kuwa na hali isiyo sahihi na hali kadhalika.

Maambukizi: Sababu ya maradhi ambayo inaweza kusambaa kutoka kwa mtu mmoja kwenda kwa mwingine, kama virusi, bakteria na vimelea.

Ugonjwa: Mkusanyiko wa dalili ambazo husababisha sehemu za mwili kuacha kufanya kazi kwa namna ya kawaida. Magonjwa yanaweza kusababishwa na maambukizi, maumbile, mtindo wa maisha au mazingira.

Mlipuko: Ni wakati watu wengi zaidi wanapoathiriwa na ugonjwa kuliko inavyotegemewa katika jamii, eneo au msimu. Mlipuko unaweza kudumu kwa siku kadhaa, wiki kadhaa au miaka.

Ugonjwa wa mlipuko: Wakati ugonjwa wa kuambukizwa unapoathiri idadi kubwa ya watu ndani ya muda mfupi, ukisambaa ndani ya jamii au nchi moja au zaidi

Janga la ugonjwa wa mlipuko: Wakati ugonjwa wa kuambukiza unapoathiri idadi kubwa ya watu ndani ya muda mfupi unapokuwa wa kidunia, au unaathiri eneo kubwa sana, ukivuka mipaka ya kimataifa na kawaida huathiri idadi kubwa ya watu.

Magonjwa yanayodhibitiwa kwa chanjo: Magonjwa yanayoweza kuzuilika kwa kupata chanjo sahihi.

Mfumo wa kinga: Mfumo wa mwili ambao kawaida hupambana na magonjwa.

Nani anakuwa katika hatari zaidi kwenye dharura ya afya ya umma?

Watu wote wanaweza kuwa hatarini kuumwa lakini wengine wapo hatarini zaidi kupata maradhi kuliko wengine au kukabiliana na “matokeo ya afya dhaifu” (kifo au matatizo ya muda mrefu). Hii inaweza kuwa kwa sababu ya:

- Tabia zao zinawaweka hatarini (mfano wahudumu wa afya au wanafamilia wanaohudumia wale wanaoumwa)
- Kinga za miili yao hazijajengeka kikamilifu (mfano watoto chini ya miaka mitano) au wanadhoofu kutokana na hali zingine (mfano wanawake Wajawazito na watu wenye hali za kiafya ambazo zinaathiri mfumo wa kinga, kama vile wazee)
- Wanashindwa kutoka kwenye maeneo yaliyo hatarishi zaidi (mfano watu wenye changamoto ya kutembea au wenye changamoto kubwa ya afya ya akili)
- Wapo dhaifu kutokana na majukumu yao ya kijinsia (mfano wasichana na wanawake, ambao wanategemewa kuhudumia wale walioathirika na ugonjwa na hivyo kuwa katika hatari kubwa ya kuambukizwa).

Jedwali lifuatalo linaonyesha baadhi ya makundi ya watu ambayo yanawezekana kuwa hatarini zaidi kudhurika au kupata maradhi wakati wa dharura ya afya ya umma, na namna ambavyo wanaweza kuwa katika hatari. Hii siyo orodha ya wale ambao wapo hatarini zaidi - watabadilika kutegemea na kilichosababisha dharura ya afya ya umma.

Zungumza na waitikijaji wa dharura pindi unapotambua wakina nani wadhaifu na wapo hatarini zaidi, kwa nini na namna gani, sababu hawa ni kundi maalumu ambalo kazi yako itajaribu kuwasaidia.

Mifano ya watu walio hatarini	Mifano ya kwa nini na namna gani wapo hatarini
<ul style="list-style-type: none"> • Wahudumu wa afya • Watu wanaosafisha taka za mwili na uchafu • Watu wanaohudumia wafu • Watu wanaohudumia wengine 	<p>Wanapokaribiana na watu wakati wanaumwa na/ au wakati wanaweza kuwaambukiza zaidi, na wao wanakuwa pia hatarini kuugua. Wafanyakazi wa afya wakati mwingine nao hulengwa wakati wa vurugu zenye silaha, na kwenye muktadha wa kibinadamu mara nyingi wao hufanya kazi kwenye mazingira hatari zaidi.</p>
<ul style="list-style-type: none"> • Watu wenye masuala ya kiafya ambayo yanadhoofisha mfumo wa kinga • Wazee • Wanawake wajawazito • Watoto, hususani walio chini ya miaka mitano na wachanga 	<p>Watu wenye mfumo wa kinga dhaifu wana uwezo mdogo wa kupambana na maambukizi ya magonjwa. Kwenye baadhi ya muktadha, ukosefu wa huduma ya afya ili kuzuia, kusimamia na kutibu msingi wa hali ya kiafya na vifo wakati wa dharura ya afya ya umma. Lishe ya chini pia ni hatarishi kwa makundi haya, kama watoto, wanawake wajawazito na wale wenye matatizo ya kiafya wanahitaji vyakula vyenye lishe ili kuishi. Kwa kuongezea, watu – hususan watoto wanaougua ugonjwa wa kuharisha mara kwa mara watakuwa chini ya lishe na pia watakuwa wana mfumo wa kinga ambao ni dhaifu.</p>
<ul style="list-style-type: none"> • Watoto • Wazee • Watu wanaoishi na ulemavu • Watu wenye changamoto ya afya ya akili • Wanawake 	<p>Watu hawa wanaweza kukutana na changamoto nyingi za ziada, zikiwemo kupatikana kwa afya na huduma zingine, kujitunza, kuwa na uwezo wa kuhama eneo ambalo limeathiriwa na dharura ya afya, na kadhalika.</p>
<ul style="list-style-type: none"> • Orang-orang dengan kondisi kehidupan yang sangat berbahaya, misalnya mereka yang terdampak langsung darurat kemanusiaan 	<p>Tazama sehemu hapo chini, magonjwa na afya dhoofu wakati wa majanga ya kibinadamu (disease and ill health in humanitarian crises).</p>

Magonjwa na afya dhoofu wakati wa majanga ya kibinadamu

Wakati wa majanga ya kibinadamu kunaweza kuwa na aina fulani ya hatari kubwa ya magonjwa na afya dhoofu kwa sababu miundo mbinu inaweza kuwa imeharibika, na kwa sababu watu mara nyingi huishia katika hali tete bila usafi stahiki.

Kupata malazi, chakula, maji safi, huduma ya afya, na msaada wa familia na jamii kunaweza kuvurugika vibaya. Sababu hizi zote zinaweza kuathiri mno afya, uwezekano wa kufanya hali kuwa mbaya zaidi na kuathirika zaidi na mlipuko wa ugonjwa.

Sababu kadhaa muhimu zinazochangia kwa magonjwa na afya dhoofu wakati wa muktadha wa kibinadamu zimeorodheshwa hapo chini:

- **Lishe:** Ukosefu wa uwezo wa kupata chakula cha kutosha na chenye lishe hupelekea lishe duni (aina ya utapiamlo). Watoto wachanga na watoto wadogo kawaida huwa wa kwanza kuathirika na hili. Upungufu wa lishe kama anemia, kukonda na kudumaa vyote hutumika kama vipimo vya lishe duni. Lishe duni na upungufu wa lishe pia hudhoofisha mfumo wa kinga, ikimaanisha kuwa mwili hauna uwezo wa kupambana na magonjwa kama unavyopaswa.

Hii inamaanisha kwamba mtu aliye na lishe duni ana uwezekano mkubwa wa kuugua na yupo hatarini zaidi kufariki kutokana na maambukizi kama kipindupindu, magonjwa ya kuharisha, mafua na homa ya mapafu. Kunyonyesha watoto ni muhimu ili kupunguza madhara ya utapiamlo, hususani kwa wale walio chini ya miezi sita; bali ili kuwa na ufanisi, mama awe anapata virutubisho vya kutosha na kama mama ana lishe duni, na mtoto anayenyonya atakuwa na lishe duni.

- **Maji:** Kutegemea na majanga ya kibinadamu, maji na mifumo ya usafi vinaweza kuharibiwa, au watu wanaweza kuwa wanaishi kwenye kambi na makazi ya muda bila miundombinu sahihi ya maji. Kwenye kesi zote mbili, upatikanaji wa maji safi, sabuni na bidhaa za usafi unaweza ukawa hafifu au haupo. Mifumo ya usafi inaweza isitengenezwe kwa muda fulani, na awali hakutakuwa na/ au vitakuwa vichache mno hasa huduma za afya na dawa. Milipuko ya kipindupindu ni hatari ya kawaida kwenye hali zenye usafi duni na usafi wa mazingira na mazingira ya kuishi yaliyobanana sana.



- **Magonjwa ya kuambukiza:** Idadi kubwa ya watu wanaoishi kwenye makazi ya muda yaliyobanana sana bila kupata maji safi, usafi wa mazingira unaostahili na mara nyingi kiwango kidogo cha chanjo hutengeneza hali ya kusambaa kwa kasi kwa magonjwa ya kuambukiza. Hii inaweza kujumuisha magonjwa ya kuharisha (ikiwemo kipindupindu), magonjwa yanayoweza kuthibitiwa kwa chanjo (kama ugonjwa wa kupooza na surua) na mafua.

Panaweza pia kuwa na idadi kubwa ya watu walioathirika kwa magonjwa yanayoambukizwa na wadudu au wanyama, kama vile malaria au homa ya dengue kwa kuwa ukosefu wa mifereji ya maji hutengeneza mazalia na makazi ya mbu.

- **Afya ya ngono na uzazi:** Kutegemea na majanga ya kibinadamu, huduma ambazo husaidia afya ya ngono na uzazi zinaweza zisipatikane. Hii inaweza kumaanisha ukosefu wa upatikanaji wa njia za uzazi wa mpango, uzazi wa mpango wa dharura, huduma ya afya ya mama na mtoto mchanga, usimamizi wa hali ya afya ya uzazi, na kuzuia na kutibu magonjwa ya ngono (STIs) na virusi vya ukimwi (HIV).

Juu

Mhudumu wa afya akimlisha mtoto kwenye kituo cha matibabu ya Ebola huko Sierra Leone.

HISANI: CARL DE SOUZA/
AFP/GETTY IMAGES

- **Afya ya mtoto:** Kuvurugika kwa huduma za afya inamaanisha kuvurugika kwa ufuutiliaji wa afya ya mtoto, msaada kwa wazazi na chanjo za watoto. Mfumo wa kinga huendelea kukua mpaka mtoto akifikisha miaka mitano. Hii inamaanisha mtoto wa miaka chini ya mitano anaweza kuumwa haraka sana na uwezekano wa kufa wakati wa mlipuko wa ugonjwa au kutokana na utapiamlo.
- **Vurugu:** Wakati wa majanga ya kibinadamu, kiwango cha dhuluma za nyumbani huongezeka, huku wanawake na watoto ndio wakiathirika zaidi. Ubakaji na unyanyasaji wa kijinsia hususan kwa wanawake na wasichana huongezeka na mara nyingi upatikanaji wa matibabu kwa majeraha, msaada wa kihisia na kiakili au uwajibikaji wa kisheria dhidi ya mtuhumiwa hukosekana.
- **Afya ya akili:** Kuenea kwa masuala ya afya ya akili kunaweza kuletwa na kushuhudia au kupitia maumivu wakati wa majanga ya kibinadamu. Mikazo wa kila siku ya umaskini, upotevu wa riziki, kutengwa na jamii kunaweza kutishia afya ya akili za watu. Mkanganyiko wa akili baada ya majanga (PTSD), sonona, wasiwasi na matumizi mabaya ya dawa ni masuala ya afya ya akili yanayojulikana kwenye muktadha huu.
- **Majeraha:** Aina ya janga la kibinadamu litaamua aina ya majeraha. Majeraha ya kujikata, majeraha ya kuungua, mifupa iliyovunjika, kuzama, kupigwa risasi, kupigwa na kutokwa damu kwa ndani, kuchomwa na ncha kali, kupoteza viungo, n.k. vyote vinahitaji huduma ya kwanza ya haraka, na vinaweza vikahitaji upasuaji mkubwa na mgumu. Watu wengi hawafahamu nini cha kufanya pindi mtu anapoumia: Hawajui hatua za haraka wanazopaswa kuchukua au jinsi ya kupata msaada na utunzaji unaopatikana.
- **Hali mbaya ya kiafya na ulemavu:** Watu wanaoishi na magonjwa yasiyo ya kuambukiza, hali mbaya ya kiafya au ulemavu wanaweza kuwa na mahitaji ya dawa za kutumia kila mara ambazo upatikanaji wake unaweza ukasita wakati wa majanga ya kibinadamu. Hii inamaanisha kwamba watu wenye kisukari, kansa, ukimwi, ugonjwa wa baridi yabisi, changamoto ya kutembea, kifafa, upofu, uziwi au magonjwa yanayohusiana na usahaulifu wana mahitaji muhimu ya ziada ikiambatana na mahitaji ya chakula, maji safi, malazi na huduma muhimu za afya.



4 Jinsi ya kuokoa maisha: Mwongozo kwa mawasiliano

Sehemu hii inaainisha baadhi ya vitu, kama mwandishi wa habari, mhariri, au mtengeneza kipindi, unavyoweza kufanya kusaidia vyema wajumbe watazamaji wakati wa dharura ya afya ya umma.

Tayarisha

Kuwa mfanisi, vyombo vya habari na uitikiaji wa mawasiliano wakati wa dharura za afya ya umma unapaswa kufanyika haraka. Matayarisho mazuri husaidia mwaitikio wa haraka. Anza kutengeneza mawasiliano na waitikiaji wa dharura, mashirika ya afya na wataalamu ambao ni wazuri katika mawasiliano. Kupalilia haya mahusiano inaweza kusaidia kuhakikisha kwamba vyombo vya habari na mawasiliano ni sehemu ya mwaitikio wa dharura na itafanya iwe rahisi kufikia hatua zingine zilizoordheshwa kwenye hiki kitabu.

Kwenye baadhi ya maeneo, mashirika kama “Msalaba Mwekundu” yanaweza yakawa yanachukua hatua za kazi za matayarisho na jamii ya eneo husika, ikiwemo kutengeneza mifumo ya kufuatilia ugonjwa na kuanzisha mipango kwa ajili ya nini bora kifanyike wakati wa mlipuko. Jadili na haya mashirika jinsi utakavyotoa msaada bora kwa ajili ya hii kazi.

Juu

Mwandishi wa habari akimhoji mfanyakazi wa “Msalaba Mwekundu” kuhusu namna na vitendo watu wanavyoweza kustahimili baada ya tetemeko la ardhi la mwaka 2010 huko Haiti.

HISANI: BBC MEDIA ACTION

Vyanzo vya taarifa vinavyoaminika

- **Mashirika yaliyojikita katika masuala ya afya:** Médecins Sans Frontières (MSF), Shirika la Afya Duniani (WHO), UNICEF, United Nations Population Fund (UNFPA), Wizara ya Afya eneo husika na Kituo cha Kuthibiti na Kuzuia Magonjwa (CDC).
- **Mashirika ya kitaifa na ya kimataifa yasiyo ya kiserikali (NGOs):** Mashirika yasiyo ya kiserikali ya eneo husika na harakati za Msalaba Mwekundu/ Red Cross.
- **Wanajamii:** Viongozi wa dini, viongozi wa kijamii, viongozi wa vijana, viongozi wa umoja, n.k.
- **Waitikiaji wa mstari wa mbele:** Inajumuisha wahudumu wa afya, wahamishaji wa kijamii, polisi na wakati mwingine maafisa wa jeshi.

Wakati wa dhurura kubwa za afya ya umma, tovuti ya ReliefWeb.int na humanitarianresponse.info zinaweza kuwa na mawasiliano na taarifa muhimu.

Fanya utafiti wako

Ni muhimu kwa waandishi wa habari kujua taarifa muhimu kuhusu dharura ya afya iliyopo – uzuiaji wake, uenezwaji na matibabu – lakini waandishi wa habari sio wataalamu. Tambua vyanzo ambavyo vinaweza kutoa taarifa sahihi na kukufundisha zaidi kuhusu hiyo mada.

Weka malengo

Kuna namna nyingi tofauti ambazo unaweza kuwasaidia watazamaji wako wakati wa dharura za afya ya umma. Kama upo wazi juu ya kile unachotaka kufanikisha kupitia kipindi chako, maudhui yako yana uwezekano mkubwa wa kufanikiwa.

Orodha ifuatayo inaainisha baadhi ya vitu ambavyo vipindi vya vyombo vya habari vinaweza kusaidia kufanyika wakati wa dharura ya afya ya umma:

Wasaidie watazamaji kuendelea kuwa na afya kwa:

- Kuwapa taarifa sahihi kuhusu kinachoendelea na kilichosabisha majanga
- Kuelezea hatua za uitikiaji wa dharura zinavyoendelea na namna ya kupata msaada
- Kuwaambia namna ya kuzuia kusambaa kwa ugonjwa na nini cha kufanya kama wao au wanafamilia wana dalili

Hamasisha watazamaji kustahimili changamoto wanazokumbana nazo kwa:

- Kutoa mifano halisi ya hadithi chanya za waliostahimili na kupona
- Kupeana uzoefu na kujifunza toka kwa wengine walioathiriwa na dharura
- Kuwapa muda wa kipindi ili kugawa mbinu zao za kustahimili na kuuliza maswali kwa wataalamu wa afya, waitikiaji wa dharura na viongozi wa kisiasa
- Kuwaalika watu wanaoaminika ili kutoa uhakika na mwongozo

Punguza unyanyapaa kwa watu walioathirika na matatizo ya kiafya kwa kuwasaidia watazamaji kwa:

- Kuamini ukweli wa kiafya kuliko ushirikina, na kusaidia kushinda miiko
- Kuwa na huruma kwa watu walioathirika na dharura na kuelewa kile wanachopitia
- Kujihisi umehamasika kusaidia wale walioathirika bila kusababisha hatari au maumivu zaidi

Kukabiliana na uvumi hatari na mitazamo isiyo sahihi kuhusu majanga ya afya kwa:

- Kutoa ukweli kutoka sauti zinazoaminika
- Kutambua na kusahihisha dhana potofu na taarifa za uongo
- Kuwaalika wajumbe wa hadhira kuuliza maswali kuhusu ugonjwa au dharura na kuelekeza maswali kwa wataalamu wanaoaminika
- Kusimamia matarajio kuhusu nini kinawezekana au hakiwezekani kufanikiwa, ili kuepuka hasira na kukata tamaa

Saidia jamii kupata huduma za afya na msaada kwa:

- Elekeza umakini kwa jamii au masuala ambayo mahitaji yake hayajafikiwa (na kuruhusu wale wanaowajibika kuitikia na kutatua matatizo).

Mifano ya taarifa muhimu

Wakati wa dharura ya afya ya umma, watu watakuwa na matamania ya kupata majibu kwa aina ya maswali yafuatayo:

- Nini kinaendelea?
- Kwa nini?
- Wapi?
- Nani yupo hatarini?
- Ni hatari gani?
- Ni namna gani ninaweza kujilinda mimi na jamii yangu?
- Nifanyeje iwapo mtu ninayemfahamu anaumwa?
- Ni aina gani ya msaada na matibabu yanapatikana, wapi na namna gani ninaweza kuyapata?
- Ni salama kwenda kwenye kituo cha afya?
- Kuna namba ya dharura – kama ndio, ni ipi?
- Ni mashirika gani yanasaidia? (elezea nembo zao, jinsi ya kuzitambua na huduma ambazo hutolewa na kila mmoja wao)
- Tunatupaje taka?
- Nini kitatokea kwa watu waliopona?
- Waliopona wanaweza kunifanya mimi au familia yangu kuumwa?
- Kutakuwa na chanjo ya kutulinda?
- Nani atawatunza watoto waliopoteza familia zao?
- Kwa muda gani dharura inaweza kuendelea?
- Tunaweza kurudi kuendelea kufanya yale tuliyokuwa tunayafanya kabla, au tunatakiwa kuendelea kufuata hatua za kuzuia?
- Kutatokea mlipuko mwingine au dharura ya kiafya kama hii? Kama ndio, tunawezaje kuizuia?
- Ni lini salama kusafiri/au kurudi sokoni/shuleni/kazini?
- Ni wapi ninaweza kupata taarifa zaidi?

Kuratibu

Wakati wa dharura ya afya ya jamii, vyombo vya habari na waitikiaji wa afya lazima wafanye kazi pamoja kuunda mrejesho wa mawasiliano ulioratibiwa ambao unatoa taarifa kwa wakati, wazi na kuaminika. Shirikiana na vyombo vingine vya habari, mashirika ya kitaifa na ya kimataifa pamoja na wafanyakazi wa serikali kutambua kinachoendelea na kutambua taarifa muhimu kwa ajili ya watu walioathirika na dharura ya afya. Kama utaratibu wa mawasiliano yaliyoungana upo, jaribu kugonga humo ili kuongeza rasilimali na kupunguza sintofahamu na juhudi za kujirudia.

Toa taarifa zenye vitendo na kutekelezeka

Maeneo yanayoguswa na vyombo vya habari wakati wa dharura ya afya ya umma mara nyingi huzingatia mapitio ya jumla juu ya hali halisi (kama vile kiwango cha dharura au idadi ya vifo) na mambo hasi (yakiwemo mateso ya binadamu, na mapungufu ya serikali na waitikiaji wengine). Lakini wakati wa majanga, watu wanaoathirika au walio hatarini wanahitaji, kuliko chochote, “habari wanayoweza kuitumia”.

Tumia muda wako wa hewani kujumuisha taarifa zenye vitendo ambazo watu wanaweza kuzitumia ili kuboresha hali zao, kama vile hatua nyepesi za kusaidia kuzuia maambukizi, nini cha kufanya iwapo atatokea mtu anaumwa na vyanzo muhimu vya kutoa taarifa zaidi na msaada. Uwe na uhakika wa kutoa maudhui kwa walioathirika, sio kuhusu wao tu.

► UTAFITI WA KUJIFUNZA

Sauti zinazoaminika

Mwaka 2012, mlipuko wa ugonjwa wa kupooza ulianza Somalia. Timu ya BBC Media Action iliwatumia washairi wanaoheshimika waliojumuisha na pia watoa chanjo na wataalamu wa afya kwenye kipindi chetu cha redio na magazeti ili kusaidia wasikilizaji kufanya uchaguzi wenye taarifa juu ya ugonjwa wa kupooza na chanjo. Washairi walitengeneza na kusoma mashairi yenye taarifa za ugonjwa wa kupooza na chanjo, wataalamu wa afya walielezea ukweli, na watoa chanjo walihojiwa ili kutoa maelezo kwa nini walikuwa watoa chanjo - kusaidia kujenga uaminifu pindi wanapotembelea jamii.

Soma hapa zaidi:

<https://www.bbc.co.uk/mediaaction/where-we-work/africa/somalia/polio-vaccination>

Tumia sauti zinazoaminika

Watu watafanyia kazi taarifa na mwongozo tu kama wanauamini, na sehemu kubwa ya kuamini inategemea taarifa inatoka kwa nani. Ni muhimu sana kuwa na watu (“sauti”) kwenye kipindi chako ambao wasikilizaji wanawaamini. Kwa kugemea jamii na muktadha, huu utakua mjumuiko wa wenye haiba inayojulikana, viongozi wa kijamii, wataalamu wa afya na watu “kama mimi” – watu ambao watazamaji wanaweza kuwashahihisha, kimtazamo wale ambao wameshafanyia kazi miongozo sahihi, na wamechukua hatua sahihi kuingia afya zao au wamepata matibabu toka vituo vya afya vilivyothibitishwa.

Hadithi binafsi

Hadithi binafsi toka kwa watu walioathirika moja kwa moja au sio moja kwa moja na dharura ya afya ya umma zinaweza kuwa na nguvu ili kuweka ukawaida uzoefu na hisia za watu kuhusu janga, kuwasaidia watu huhisi wanasaidiwa na hawajatengwa, na kujenga huruma kwa wengine. Hadithi binafsi husaidia watu kutambua kuwa sio wao pekee wanaokumbana na janga na kwamba kuna wengine wanahisi na wameshaitikia namna hiyo. Maelezo binafsi pia huonyesha kwa wasikilizaji jinsi watu kama wao walivyoweza kushinda changamoto na kuanza tabia mpya. Hakikisha unajumuisha sauti za watu kutoka kwenye jamii unayotaribu kuilenga, kama vile watoa matunzo majumbani, na pia wale watu walio kwenye mazingira magumu waliopuuzwa, kama vile wazee au watu wenye ulemavu.

Kuingiliana

Muingiliano wa watazamaji ni muhimu kwa vipindi vyenye ufanisi. Na pia kwa kufanya vipindi vivutie na hai, hii huleta watu pamoja na kusaidia watazamaji kukua kutoka kufahamu kuhusu dharura ya afya na kupelekea kuwahamasisha kuchukua hatua ya kuuzuia usiathiri zaidi.

Muingiliano wa watazamaji:

- Huwapa watu jukwaa la kutoa mahitaji yao na kuibua maswali na wasiwasi wao
- Hutengeneza hisia ya ujamaa na muunganiko
- Huimarisha hisia ya umma ya umiliki
- Husaidia kutambua mapengo kwenye muitikio wa wakati wa dharura na kuwashikilia mamlaka kuwajibika
- Husaidia kutambua na kusahihisha taarifa za uongo
- Huwezesha mtiririko wa taarifa kati ya wataalamu na watu
- Husaidia watu kupeana uelewa na elimu ambayo itawaongoza kuchukua hatua sahihi
- Huondoa unyanyapaa kwenye hali ya kiafya kwa kuwaweka watu kawaida, na kujenga uelewa na huruma
- Huweka ubinadamu kwenye vipindi vyako na masuala yaliyomo, kuvifanya viwe shirikishi zaidi
- Inakuwezesha kuzidi kuwajua wasikilizaji wako vizuri na kupokea taarifa na maudhui toka kwao

Kuchangamana na watazamaji

Fikiria namna utakavyoweza kutumia mifumo yako iliyopo kutengeneza mijadala na ushirikishwaji wa watazamaji. Haya ni baadhi ya mawazo:

- Kipindi cha kupiga simu (mfano kipindi cha maswali na majibu kwa mtaalamu kuhusu dharura za kiafya)
- Kipindi cha maswali na majibu kwenye mitandao ya kijamii (mfano Facebook)
- Majaribio ambayo wasikilizaji wanaweza kushiriki kupitia kutuma ujumbe mfupi wa maneno au kupiga simu
- Wasikilizaji kutoa hadithi zao binafsi*
- Vox pops*
- Mijadala mubashara inayofanyika kwenye ukumbi
- Mahojiano na watazamaji*

* **Usiwalete watu pamoja kwenye nafasi, au kufanya mahojiano au vox pop binafsi, kama janga la kiafya linaunganishwa na ugonjwa wa kuambukiza na kuna hatari ya kiusalama.** Badala yake, endesha mahojiano kwa simu au tovuti kama Skype au Apps za kutuma ujumbe. Tafuta ushauri kwa wataalamu kabla ya kukutana ana kwa ana na watu muhimu walioathirika.

Pia zingatia:

- Ni njia gani ya mawasiliano (mfano simu) ambayo watazamaji wako tayari wanayo ambayo itawawezesha kuingiliana na vipindi vyako? Je, kila mtu anavipata, au ni sehemu tu ya wasikilizaji wako? (mfano walio na uwezo wa kifedha zaidi)?
- Una rasilimali za kutosha kuitikia au kusiamamia aina yo-yote ya uingilianaji wa watazamaji? Uingiliano wa watazamaji unaweza kuwa na uhitaji wa nguvukazi kubwa, kama kuhitaji watendakazi kupokea simu au kusafiri kwenda kufanya vox pop
- Ni masuala gani ya usalama unapaswa kuzingatia (mfano umri na wenye uwezekano mkubwa wa kupatwa na matatizo fulani) ya watazamaji wako na usalama wa wafanyakazi wako)?
- Unaweza ukahitajika kulinda utambulisho wa wasikilizaji ambao wanachangia?
- Kuna namna yo-yote ya kuhakikisha kwamba wenye uwezekano mkubwa wa kupata matatizo (mfano wazee, watoto, wasichana na wanawake na watu wenye ulemavu) wanaweza kuchangamana na/au wakawakilishwa vyema kwenye kipindi chako?

Wazingatie watu walio katika uwezekano mkubwa wa kupata

Wakati wa dharura yo-yote ya afya ya umma, watu walio kwenye uwezekano mkubwa wa kupata matatizo ni wale walio katika hatari zaidi ya matatizo ya afya na wale walio na uwezo mdogo wa kujitunza. Kama ilivyoelezwa kwenye sehemu ya 3, hii inaweza kujumuisha watoto, wazee, wanawake na wasichana (hususan wanawake wajaawazito), watu wenye ulemavu, na watu walio na matatizo ya afya na masuala ya uzima.

Katika kupanga kipindi chako, zingatia mahitaji maalum ya haya makundi ambayo mara nyingi ni makubwa kuliko, au yanaweza kuwa tofauti na yale ya wengine

- Mahitaji gani waliyo nayo?
- Ni kwa namna gani mahitaji haya yatafikiwa?
- Ni ulinzi na msaada gani wanaohitaji?
- Nani anawatunza na msaada gani wanaohitaji wanaowatunza?

Kabiliana na uvumi

Pambana moja kwa moja na hadithi na mitazamo potofu kuhusu maambukizi au ugonjwa katika kiini cha janga la kiafya – visababishi vyake, maambukizi, kuzuia, matibabu na unyanyapaa kwa watu walioathirika.

I Tambua

Sikilizia uvumi na taarifa zisizo sahihi, ambazo zinaweza kusambaa kwa haraka kwa njia ya mdomo na kwa haraka zaidi kwenye mitandao ya kijamii.

►UTAFITI WA KUJIFUNZA

Vipindi vya kuchangamana

Wakati wa mlipuko wa 2014–2016 Afrika Magharibi, moja ya vipindi ambavyo BBC Media Action walitengeneza ni majadiliano ya redio na kipindi cha kupiga simu. Wageni waalikwa wakiwa ni wataalamu wa afya, wasikilizaji waliweza kupiga simu kuuliza maswali kuhusu mlipuko, mabadiliko yanayotakiwa katika vitendo vya kitamaduni ili kuzuia kusambaa kwa Ebola, na uvumi waliosikia. Watu waliweza kuuliza maswali waliyohitaji majibu, kupeana uzoefu na kupata ufafanuzi wa moja kwa moja juu ya kilichokuwa kinaendelea, virusi vya Ebola, na kwa nini baadhi ya vitendo vya kitamaduni vilihitajika kubadilika au kuachwa.

Soma zaidi hapa:

<https://www.bbc.co.uk/mediaaction/where-we-work/africa/sierra-leone/sierra-leone-ebola-response>

2 Hakikisha

Ukikutana na uvumi au taarifa zenye utata ambazo zimesambaa kwa mapana, hakikisha kuhusu ukweli wake.

3 Zingatia

Fikiria kuhusu maana ya uvumi – unaweza kuleta madhara ya moja kwa moja au vinginevyo?

4 Sahihisha

Kama uvumi ukisambaa kwa mapana unaweza kuleta madhara, inabidi kukabiliana nao kwa taarifa sahihi. Kupamabana na hadithi na dhana potofu, kwa kawaida utahitajika kufanya zaidi ya kutoa maelezo ya kawaida kuwa sio sahihi. Hakikisha una vyanzo vinavyoaminika ambavyo vinaweza kujadili na kuelezea kwa uwazi na ukweli kwa namna ya kujali na kuheshimu. Changamana na wasikilizaji na waalike kuuliza maswali ili kuwasaidia kuamini ukweli na kutambua taarifa zisizo sahihi hapo mbeleni.

Kwa mwongozo wa ziada juu ya uvumi, tazama hii: *Communicating with Disaster-Affected Communities (CDAC) Network*:
<http://www.cdacnetwork.org/tools-and-resources/i/20170613105104-5v7pb>

►UTAFITI WA KUJIFUNZA

Kukabiliana na uvumi

Juhudi ya kupambana na ugonjwa wa kupooza Afghanistan kwa miaka ya karibuni umekuwa ukikandamizwa na uvumi wa uongo kuhusu chanjo ya ugonjwa wa kupooza. Kumekuwa na madai kwamba si halali na kwamba imetengenezwa kwa mkojo wa wanyama na kwamba inadhuru watoto kwa kuwaharibu vizazi. Wahudumu wa afya na mamlaka wamekuwa timu na viongozi wa Kiislamu na viongozi wa kijamii kuwashawishi watu kwamba chanjo ni salama. Wamechukua Fatwas (sheria za kidini) toka kwa wasomi wa dini wenye ushawishi kwa maandishi na video, kusaidia kuwashawishi wazazi wasioelewa kwamba chanjo ya ugonjwa wa kupooza inaruhusiwa kwenye dini ya Kiislamu.

Soma zaidi hapa:

<https://www.thenewhumanitarian.org/feature/2018/05/10/afghanistan-battles-polio-rumours-mistrust-and-negotiating-taliban>

Kuwasiliana vyema

Ili kufanya mawasiliano na vipindi vyako kuwa vya kufikika, vya kujenga na vya msaada kadri iwezekanavyo, ni muhimu kuhakikisha vinafikia vigezo vifuatavyo:

- **Wazi:** Ondoa vifupisho, misamiati na lugha za kitaalamu. Baki na lugha ambayo watu wataelewa. Mara zote elezea neno lo-lote ambalo linaweza kuwa halitambuliki au halipo wazi kwa watazamaji.
- **Sahihi:** Patia! Kuwa na taarifa za wakati na jifunze kuhusu masuala husika ya kiafya. Usichangie kwenye hadithi na dhana potofu ambazo zinaweza kuwa kikwazo kwa juhudi za kuzuia. Kama taarifa zako zitatazamwa kama si sahihi au hazijakamilika, utapoteza imani ya watazamaji wako na inaweza kusababisha kutokea madhara mabaya kuliko mazuri. Fikiria madhara ya kawahakikishia watu kuwa chanjo inafika kesho, wakati ipo katika ya majaribio na haitaweza kupatikana kwa mtu yo-yote kwa muda wa zaidi ya wiki au miezi kadhaa. Ukiwasilisha taarifa zo-zote zisizo sahihi, rekebisha mapema iwezekanavyo na wataarifu mamlaka husika ili waweze kudhibiti madhara yake.
- **Kuaminika:** Onyesha kuwa unajali kuhusu hali nzuri ya watazamaji wako na kujaribu kuwasaidia. Fanya kazi na wanajamii wanaoheshimika ili kusaidia kuwasilisha taarifa muhimu. Usizitumie hadithi zao za mateso.
- **Thabiti:** Ratibu na wawasilianaji wengine, kama viongozi wa kijamii na waitikiji wa mstari wa mbele, kuhakikisha kuwa hutoi taarifa zinazokinzana kwa watu. Kama kuna kukosekana kwa uthabiti katika ujumbe, tafuta sababu ya kwa nini na lenga kuzisahihisha.
- **Suluhisho lililo na malengo:** Wasaidie watazamaji kutafuta suluhisho kwa changamoto zinazowakabili. Tambua vikwazo vya kufikia kuzuia na kutibu ugonjwa, na jadili unyanyapaa dhidi ya mtu ye-yote mwenye dalili. Zungumza kuhusu hofu walizo nazo watu na chunguza suluhisho inayowezekana, kama vile kutambua na kujadili mijadala ambayo ni ya kijamii ili kukabiliana na matendo ya kitamaduni ambayo yanapelekea uhatarishi.



- **Ya ukweli:** Kama watu kwenye jamii hawana sabuni na hawawezi kupata, usiwaambie waoshe mikono yao kwa sabuni. Dadisi ni kitu gani wanaweza kutumia badala yake (mfano majivu) na toa hiyo kama chaguo. Ni hatua gani rahisi na zinazoweza kufanyika ambazo zitawasaidia watu kuhisi wana uwezo kiasi wa kuyatawala majanga?
- **Vitendo:** Saidia kusimamia mahitaji na kupatikana kwa huduma za afya na mwitikio wakati wa dharura. Tambua aina ya huduma zinazopatikana (kama namba za simu za msaada, vituo vya matibabu na vituo vya upimaji) na kuwa wazi juu ya wakati gani na namna watu wanavyoweza, na wanavyopaswa, kuvipata. Kwa mfano, watu wanaweza kufaidika na huduma ya upimaji baada ya kuonyesha dalili fulani pekee au baada ya kuwa kwenye mazingira fulani ya hatari, au namba za simu za msaada zinaweza kufanya kazi wakati wa masaa ya mchana tu.

Above

Kumbuka kuonyesha huruma unapozungumza na wana-jamii.

HISANI: BBC MEDIA ACTION

- **Yenye huruma:** Tia ubinadamu kwenye maudhui yako. Tekka hisia za watu na waambie hadithi binafsi au wahudumu wa afya, wahamasishaji wa ufahamu, watu walioathirika na dharura za afya na wale waliowahi kuokoka hiyo dharura. Kuwa na maradhi haipendezi na wakati mwingine hutisha. Kuwa aliyeokoka wakati mwingine hutisha, na hofu ya unyanyapaa na kukataliwa na familia na wanajamii. Hii pia kwa wahudumu wa afya, ambao wamewahi kuvamiwa na kuuawa kwenye baadhi ya maeneo yaliyokumbwa na dharura ya kiafya ya umma. Waruhusu watu kuzungumzia hofu walizo nazo.
- **Inayohusisha:** Kamata umakini wa wasikilizaji wako na wawezeshe kushiriki kwenye kipindi chako. Wanaweza kutengeneza uchovu wa kusikiliza habari za masuala ya afya, hasa kwa maeneo ambayo yako hatarini lakini bado hayajaathirika. Tafuta namna mpya za kuwafanya waendeleo kusikiliza na kuzungumza kuhusu hayo masuala bila kuleta hofu (angalia mitindo mbalimbali chini).
- **Chanya:** Jaribu kutokaa kwenye hasi za dharura ya kiafya. Ni rahisi sana kukuza hofu na mihemko. Ingawa uingizaji wa mawasiliano ambao hutumia hofu na mshtuko kama mbinu huweza kuleta uelewa zaidi kwa watu, unaweza pia kupelekea unyanyapaa na kujikataa, na kuzuia mabadiliko ya tabia yanayohitajika kuzuia dharura za kiafya.

Chunguza miundo tofauti

Fikiria kwa ubunifu kuhusu njia tofauti za kuwasilisha taarifa kwa anuai ya miundo na sehemu. Kwa mfano, **‘spots’** fupi zenye mtindo wa kimatangazo zinaweza kusaidia kwenye kuwasiliana na kuongeza vipande vyepesi vya taarifa, kama “hii ndio namba ya kupiga kama una dalili hizi”. Nyimbo zinaweza kuwa namna ya kuburudisha ya kurudia ujumbe mahususi kwa namna ambayo watu watakumbuka.

Vipande virefu ni vizuri kwa kuwasaidia watu kukumbuka kile wanachopaswa kufanya, na pia kuelewa kwa nini na namna gani ya kufanya haya. Pia vinasaidia kushughulikia mada ambazo ni ngumu, nyeti au mwiko. Anuai kama mahojiano, mijadala na maigizo vinaweza kukuruhusu kuchunguza maelezo ya suala na kuwapa ubinadamu wale walioathirika kwa/au wanahusika kutatua janga la kiafya.

Uliza watu sahihi maswali sahihi

Kuwa na uwezo wa kuwa na wazamaji kwa upana zaidi katika vyombo vya habari ni kifaa chenye nguvu sana ambacho kinaweza kuwa na faida au madhara. Ni jukumu letu kuhakikisha tunachorusha hewani kinatumika kwa mema. Ni muhimu kuchagua wahojiwa sahihi kufikia mahitaji ya wasikilizaji. Chagua watu wenye uelewa sahihi, wa kuaminika na wenye uwezo wa kujieleza kwenye hilo somo. Kwenye baadhi ya kesi, mhudumu wa afya ya jamii au mtu anayepona ugonjwa anaweza kuwa wa thamani zaidi au mhojiwa sahihi kuliko kiongozi wa juu wa kisiasa. Uliza maswali ambayo yatapelekea kupata ushauri wa wazi au suluhisho na siyo taarifa za utata ambazo watu hawawezi kuzifanyia kazi.

Mifano ya maswali ya mahojiano

Maswali ya kuwauliza wataalamu wakati wa mahojiano wakati wa mlipuko wa mafua yanaweza kujumuisha yafuatayo (haya yanaweza kutumia dharura zingine za kiafya):

- Mafua ni nini?
- Yanasambaaje?
- Mtu anajuaje kama ana mafua?
- Mtu anapaswa afanyeje iwapo akidhani yeye au mtu mwingine ana mafua?
- Wapi na namna gani wanaweza kupata msaada kama wanadhani wana mafua?
- Kuna uwezekano kiasi gani wa kupona kama ukipata mafua?
- Kuna tiba ya mafua?
- Ninawezaje kusaidia kuzuia ugonjwa wa mafua usisambae?
- Ninawezaje kumsaidia mtu wakati anapona?

Usilete madhara

Wakati mwingine, wakati unajaribu kusaidia wakati wa dharura ya majanga ya afya, vyombo vya habari vinaweza kusababisha madhara zaidi bila kujua. Pamoja na kuhakikisha taarifa unayotoa ni ya ukweli sahihi, unahitaji kuzingatia matokeo ya kile unachowasilisha na namna kinavyoweza kutafsiriwa.

Kwa mfano, kwenye baadhi ya dharura, watu wanaweza wakawa hawana uwezo wa kupata maji ya kunywa, kwa hiyo mashirika ya msaada yanagawa vidonge vya krolini.

Watu wanaambiwa wanahitaji kutumia vidonge hivi ili viweze kuwalinda dhidi ya magonjwa. Lakini kumekuwa na kesi ambapo watu hawajaambiwa jinsi ya kuvitumia hivyo vidonge, kwa hiyo badala ya kuviyeyusha kwenye kiasi cha maji kinachotakiwa, wamevika hivyo vidonge, kupelekea kuhatarisha afya zao. Kukosekana kwa taarifa za kujitosheleza kulileta madhara zaidi kuliko kusaidia.

Hakikisha unaelewa maneno, matamshi au taarifa zinazoweza kutoeleweka au kutumika kunyanyapaa wengine na jaribu kuepuka hii. Kwa mfano, tumia “mtu aliyeathirika” kuliko “mhanga” na epuka kulaumu watu kwa kuusambaza ugonjwa. Badala yake, tumia lugha kama “kusambaa kwa/au “maambukizi ya” ugonjwa. Usiunganishe kikundi fulani na kusababisha au kusambaa kwa tatizo la kiafya. Hakikisha watu wanaelewa namna ugonjwa unavyoweza kumuathiri mtu na kwa kiasi gani watu wanaweza kugusana bila kunyanyapaliwa au kuwatenga.

Kama mtu au wawapendao wameathirika kwa maradhi haya, kuwa na hisia. Wanaweza kuwa dhaifu kimwili au kiakili kama wanapona ugonjwa mbaya au kuomboleza kifo cha ndugu. Jedwali kwenye ukurasa unaofuata lina baadhi ya miongozo inayofaa.

Kuwahoji watu walioathirika na dharura ya afya ya umaa

Kabla ya kuzungumza na watu moja kwa moja au isiyo ya moja kwa moja

Kama una mpango wa kuzungumza na mtu aliyeathiriwa na dharura ya kiafya, usijiweke wewe au wenzio hatarini. Kwanza, tafuta ushauri kutoka kwa mamlaka au wataalamu wa afya juu ya usalama wa kufanya hivyo na hatua zo-zote za kujilinda zitakazokuwa zinaweza kuhitajika.

Kama ukipanga kufanya huo mjadala, tayarisha kwa kuzungumza na wafanyakazi wa msaada kuhusu aina ya maswali na changamoto ambazo watu walioathiriwa na majanga ya kiafya wanayokumbana nayo na jinsi ya kuzungumza nao wakati wa mahojiano.

Mahojiano ya awali: Kuwa na mazungumzo kuhakikisha mhojiwa anajua ni masuala gani yanaweza kujadiliwa na yupo huru kuyazungumza.

Wakati wa mahojiano: Hakikisha unapata ridhaa rasmi kutoka kwa wahojiwa kabla ya kuanza mahojiano, ili watambue kwa nini wanahojiwa na namna gani yaliyomo kwenye mahojiano yatumika. Wanaweza wakahitaji watu pamoja nao kama watoa msaada wa kimaadili wakati wa mahojiano.

Mahitaji ya mtu aliyeathirika kwa dharura ya afya ya umma siku zote ni muhimu zaidi ya mahitaji ya mhoji. Kama mhojiwa akichoka sana au mwenye huzuni, au akataka kuacha mahojiano, heshimu haja zao.

Fikiria kwa mapana

Dharura za kiafya huathiri zaidi ya afya za watu. Riziki zao, elimu, shughuli za kawaida, upatikanaji wa chakula na huduma za afya za kawaida vinaweza vyote vikaathiriwa na majanga. Jaribu kuchunguza masuala ya aina hii kwenye kipindi chako pia.

Kama dharura ya kiafya ikitokea ndani ya janga la kibinadamu, kuna uwezekano wa kutokea matatizo ya kiafya kadhaa yatakayohitaji kutatuliwa, pamoja na masuala mengine yote ambayo watu wanapitia (kama kupoteza wanafamilia, makazi, risiki, na kupitia hali ya kiwewe).

5 Vyanzo vya taarifa za ziada

Uwezo shirikishaji wa mawasiliano ya afya (HC3)

https://healthcommcapacity.org/hc3-project-materials/?fwp_health_area=emergency-preparedness

Shirika la Afya Duniani

Rasilimali wakati wa dharura:

<http://www.who.int/emergencies/en/>

Mwongozo wa kuwasiliana wakati wa dharura:

<https://www.who.int/risk-communication/guidance/download/en/>

Médecins Sans Frontières (MSF)

<https://www.msf.org.uk/issues>

Kituo cha kuthibiti magonjwa (CDC)

<https://www.cdc.gov/>

BBC Media Action miongozo ya mawasiliano kwa afya na dharura zingine:

The Pulse:

<https://bbcmiaactionilearn.org/course/view.php?id=138>

Mchanganyiko wa matokeo ya tafiti juu ya utangazaji wakati wa dharura:

<https://www.bbc.co.uk/mediaaction/publications-and-resources/research/reports/Humanitarian-broadcasting-in-emergencies-synthesis-report-2015>

Chapisho hili lilitengenezwa na BBC Media Action kwa ajili ya Shirikisho la Kimataifa la jamii ya Msalaba mwekundu na Red crescent. Hili liliwezekana kwa msaada wa uliotolewa na Taasisi ya Afya Duniani, Shirika la Maendeleo ya Kimataifa la Marekani, chini ya masharti ya PIO Grants GHA G 00 08 00006 and AID GH IO 17 00002.

© BBC Media Action 2020

Kwa taarifa zaidi tafadhali wasiliana:

Tel +44 (0) 20 7481 9797

Fax +44 (0) 20 7488 9750

Email media.action@bbc.co.uk

Web bbcmediaaction.org

Ofisi iliyosajiliwa

BBC Media Action
Broadcasting House
Portland Place
London W1A 1AA
United Kingdom

Namba ya hisani zilizosajiliwa (England & Wales): 1076235